**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

Shule ya Sekondari Makiba

S.L.P 13818,

Arusha

Tarehe……………

Namba za simu

Mkuu wa Shule **0754630571/0787847981**

Makamu Mkuu wa Shule **0754 233280**

**KUMB.NA.MSS/K.5/2021**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………

S.L.P ……………………..

……………………...

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKIBA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA MERU MKOA WA ARUSHA MWAKA 2021.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2021 Tahasusi ya (i) **CBG…** ….(ii) **HGL…….** Shule ya Sekondari Makiba ipo umbali wa kilometa **53** Kusini/Mashariki mwa Jiji la **ARUSHA** kusini mwa mji Mdogo wa Kikatiti barabara ya Moshi - Arusha. Usafiri wa basi kutoka jijini Arusha unapatikana katika kituo cha mabasi (Stendi Kuu ya Mabasi). Kwa utaribu ufuatao:
   - Kwa wale ambao watakaoshukia kituo kikuu cha mabasi Arusha mjini nauli kutoka Arusha mjini mpaka Mirerani ni shilingi **3,000/=** na kisha kupanda pikipiki kutoka Mirerani mpaka shuleni kwa shilingi **3,000/=**
   - Au unaweza kusafiri kutoka Arusha mjini mpaka Kikatiti kwa shilingi **1,000/=** tu. Na kutoka Kikatiti kwa kupanda pikipiki kuja Makiba kwa shilingi **5,000/=**
   - Au unaweza kusafiri kutoka Arusha mjini mpaka KIA kwa shilingi **1,500/=** tu na kisha kupanda daladala kutoka KIA kwenda Mirerani kwa shilingi **1,000/=** tu. Na baadae kupanda pikipiki kutoka Mirerani mpaka shuleni kwa shilingi **3,000/=**
   - Na kwa wanaotokea mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Kilimanjaro wanashauriwa kushuka kituo cha KIA kisha utapanda daladala kwenda Mirerani kwa shilingi **1,000/=**.Kisha utapanda pikipiki kwenda shuleni kwa shilingi **3,000/=**

Unaweza kuwasiliana kwa namba za simu upate maelezo zaidi.
Muhula wa masomo unaanza tarehe **05/07/2021** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni

Tarehe **05/07/2021** kuanzia asubuhi saa **2:00** mpaka saa **10:00** jioni. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/07/2021**

Scanned with CamScanner

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:-**

**2.1 SARE YA SHULE (SCHOOL UNIFORM)**

a) Mashati mawili (2) meupe, yenye mikono mirefu yasio na maridadi yasiyoonesha ndani (non trasparent) nasio la kubana mwili.

b) Suruali mbili (2) rangi NYEKUNDU yenye marinda mbili (2) (suruali za ***mnyonyo*** haziruhusiwi kabisa ikikamatwa itaharibiwa)

c) Sweta rangi NY EKUNDU.

d) Nembo ya shule kwenye mashati inachapishwa shuleni kwa gharama ya shilingi 2,000/=

e) Tai rangi NYEKUNDU iwe ndefu kiasi.

f) Sare ya michezo ni rangi NYEKUNDU (Tisheti, kaptula na soksi) pamoja na viatu vya michezo

g) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi visivyo na urembo, vinapakwa rangi. viatu vyenye visigino virefu, visivyo na soli, ama vya plastic havitakiwi. Atakayekiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.

h) Soksi jozi mbili nyeusi.

i) Mkanda wakuvalia suruali ni mweusi wa ngozi usio na balkon kubwa isiyokuwa na picha yeyote

k) Nguo za kushindia (shamba dress) T'shirt ya rangi ya bluu shingo ya mduara isiyo na maandishi yeyote na suruali ya rangi ya bluu.

**2.2Ada na michango ya shule:-**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000.00** na unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000.00** kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. Shilingi **15,000/=**kwa ajili ya ukarabati wa samani.

ii. Shilingi **6,000/=**kwa ajili ya kitambulisho na picha.

iii. Shilingi **20,000/=** kwa ajili ya taaluma kwa mwaka.

iv. Shilingi **30,000/=**kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine kwa mwaka.

v. Shilingi**10,000/=**kwa ajili ya huduma ya kwanza. Tshs**5,000/=** na Bima ya afya (CHF) Tshs**. 5,000/=** kwa wale wenye bima ya afya ya taifa atalipia huduma ya kwanza tu.

***vi.*** Shilingi **20,000/=** *mitihani ya kujipima mock.*

vii. Fedha ya tahadhari **5,000/=** na fedha hii hairejeshwi.

Viii Shilingi **10,000/=**kwa ajili ya maji.

Jumla ya ada na michango yote nishilingi **188,000/=**

**NB: ADA TSH. 70,000/=** NA MICHANGO MINGINE YOTE TSH.118,000/= **ILIPWE KWENYE AKAUNTI:**

***MAKIBA SECONDARY – DEVELOPMENT ACCOUNT 40801200258 NMB*** *..JUMLA YA ADA NA MICHANGO NI TSH.188,000/=*

TAFADHALI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE *PAY IN SLIP*

Scanned with CamScanner

## c) MAHITAJI YA LAZIMA UNAYOTAKIWA KULETA

i. Ream ya karatasi 1 kwa mwaka aina ya NOPA au ROTATRIM.

*ii.* Vitabu vya masomo hivi ni kwaajili ya kumsaidia mwanafunzi kwenye masomo yake ya binafsi

- ***A.E.Tungilayo (2013) General Study Secondary Education. Mikumi Publishers Dar es salaam*** (kitabu hiki kitatumiwa na wanafunzi wamichepuo yote).

- kwa wale wa masomo ya sayansi vitabu ni:
  - GENERAL CHEMISTRY
  - PHYSICAL CHEMISTRY
  - ORGANIC CHEMISTRY
  - BIOLOGICAL SCIENCE
  - INORGANIC CHEMISTRY
  - Pamoja na vitabu vya Jiografia na BAM

- Kwa mchepuo wa Sanaa (HGL) kila mwanafunzi atakuja na vitabu vya History, Jiografia na kiingereza

iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology.

iv. Scientific calculator.

v. Laboratory coat kwa wanafunzi wa CBG

vi. Mathematical set, kalamu za wino (bluu/nyeusi ball pens za kumtosha), penseli na vifaa vingine vya kujifunzia.

vii. Madaftari (counter books) ya kutosha masomo 10.

viii. Jalada (File cover) mawili ya plastiki kwa ajili ya kufungulia faili na la kutunzia mitihani na majaribio yako.

ix. Kamusi kubwa ya kingereza (Dictionary) kati ya Oxford au Cambridge.

x. Begi au mfuko mzuri wa kuwekea vifaa vya shule.

*xi.* Sanduku imara la kuhifadhia mali yako. Tutapokea sanduku moja tu ***'TRANKA'***

*xii.* Mahitaji yote yabafuni mfano sabuni, mafuta, mswaki, taulo n.k.

xiii. Godoro futi 3 kwa 6

xiv. Mashuka pair 2, foronya 1(vyote hivi rangi ya bluu bahari) blanket1 na chandarua 1 rangi yoyote vyote viwili.

xv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

xvi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

xvii. Kwanja 1, jembe 1, mifagio ya ndani (soft bloom) na nje (chelewa) na skuiza kwa ajili ya usafi.

xviii. Ulete result slip shuleni

Scanned with CamScanner

## SHULE YA SEKONDARI MAKIBA

### SHERIA ZA SHULE

**Kaulimbiu ya shule yetu ni:** ***MBELE DAIMA NYUMA MWIKO.***

Lengo letu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri na hivyo kumwezesha Kufanikisha lengo la alichokifuata hapa. Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya AMANI, UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia bora. Kila mwanafunzi aje na nia ya KUSOMA KWA BIDII na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya MAKIBA SEKONDARI.

Kwa upande wa shule sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU Tutajitahidi kuishi, kumfundisha na kumlea mtoto lakini tutashindwa katika kazi hii bila ushirikiano mzuri wa wazazi /walezi.

Vifuatavyo ni vifungu muhimu vya sheria za shule. Kila mmoja anapaswa kuzifuata kwa ukamilifu.

- Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni kiingereza tu.Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo.
- Kwa vile shuleni ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na ukimya hasa sehemu za madarasani.
- Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama ratiba ya shule inavyoonyesha. Kazi za mikono ni moja ya elimu inayotolewa hapa shuleni. Kila mmoja lazima ashiriki bila utegaji.
- Hairuhusiwi kupeleka chakula nje ya bwalo la chakula kama bwenini. Wapo wahusika watahakikisha kuwa wagonjwa wanapelekewa chakula. Mwanafunzi haruhusiwi kuleta chakula cha aina yeyote arudipo shuleni toka likizo au arejeapo baada ya kupata kibali kutoka nje. Hii ni kwa ajili ya afya yako.
- Mavazi yote ya binafsi hayahitajiki hapa shuleni, kwa ndani ya shule muda wote ni kuvaa sare na nguo za kushindia tu (shamba-dress) isipokuwa muda wa michezo ambapo atavaa sare za michezo.
- Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa bwenini ya aina yoyote. Kwa mwanafunzi Mwenye dawa atoe taarifa kwa Patroni ili ziweze kuhifadhiwa. Wanafunzi haruhusiwi kupeana dawa bwenini.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vyombo vya muziki kama vile radio,
- Walkman, earphone na headphone vitu kama vile kamera n.k.
- Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuwa na simu au kumiliki simu.
- Wizi, matusi na ugomvi haviruhusiwi kabisa shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki silaha au kuwa na vitu vya hatari vya ncha kali kama vile visu, nondo, rungu n.k.
- Kila mmoja ana wajibika kuvitunza vifaa vyote vya shule vya shule atakavyokabidhiwa na alivyokabidhiwa kwa uangalifu wa hali ya juu vifaa vyote vya shule atakavyokabidhiwa na asivyokabidhiwa. Uharibifu au upotevu wowote utakaotokea, gharama za matengenezo au fidia zitalipwa na atakayefanya uharibifu huo.

Scanned with CamScanner

- Kila **IJUMAA**, **JUMAMOSI** na **JUMAPILI** wale waendao kusali kwenye madhehebu
  mbalimbali watavaa sare za shule na kurudi baada ya sala zao kukamilika wahi kurudi na kuendelea na ratiba ya shule.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu watu wote hapa shuleni pamoja na uongozi wa shule na uongozi wa wanafunzi atumie lugha safi kwa watu wote na atatoa matatizo yake kwa viongozi wake kwa kufuata utaratibu husika.
- Ni marufuku mwanafunzi kwenda nje ya shule ama kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi wa shule bila kibali
- Mwanafunzi ataenda kununua mahitaji kwenye duka la shule muda wa mapumziko tu.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi.
(ii) Kutohudhuria masomo kwazaidi ya siku 90 bila aarifa/ utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwaujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au namtu yeyote Yule.
(vi) Kufuga ndevu.
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa.
(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xi) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xii) Kutembelea majumba ya starehe au nyumba za kulala wageni.
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiv) Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatanisho na Fomu Muhimu.**

a)Fomu ya Uchunguziwa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b)Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c)Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d)Michoro ya muonekano wamavazi sare za shule jinsi zitakavyo shonwa.
e)Picha nne za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

***Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**Saini ya Mkuu wa Shule ..........................................**

MKUU WA SHULE
MAKIBA SEKONDARI

Jina la Mku uwa Shule.................. F.B LASWAY

MKUU WA SHULB

Mhuri wa Mkuu wa Shule ..............................

MAKIBA SEKONDARI

*Kumbuka* Shule haitoi mlo maalumu (special diet) kwa wale wote wenye matatizo ya kiafya/magonjwa sugu

*Kama hujaripoti shuleni hadi ifikapo tarehe 18 Julai 2019 utahesabiwa kuwa umeikataa nafasi hii.*

*Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia darasani bila kulipa ada namichango mingine yote . Hakikish unatimiza mahitaji yote kuepuka usumbufu usio wa lazima.*

Scanned with CamScanner

## SHULE YA SEKONDARI MAKIBA

## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

## HABARI ZA MZAZI/ MLEZI

1.Jina kamili la baba…………………………………………..
2.Kazi yake……………………………………………………………
3.Jina kamili la Mama……………………………………….
4.Kazi yake………………………………………………………………
5.Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)…………………………………………………
6.Kazi na Anwani ya Mzazi /Mlezi…………………………………………………………………………
7.Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) au 'Place of Domicile'
Kijiji/Mtaa……………………………………..Wilaya……………………………..
Kata……………………………………………… Mkoa……………………………………
Tarafa…………………………………………..

8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba……………………………………………………………………………

9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama…………………………………………………………………………

10. Mtoto anaishi na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazaziwote (iv) Walezi

* Kata isiyohusika*

11. Dini ya baba………………………………………… Dhehebu……………………………………

Dini ya Mama ……………………………………..Dhehebu………………………………….

Dhehebu analotoka mwanao…………………………………………………………

12. Anwani kamili ya nyumba ambapo motto atakuwa anakwenda siku za likizo ………………………

13. Mimi ………………………………………… (Baba/Mama/Mleziwa ……………………

Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo

Tarehe ………………………………………..                ……………………………………

Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi

Scanned with CamScanner

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII**

Mimi………………………………………………………………………. ( jinakamili)

Kidato cha……………………………………………… mwaka ……………………

Nakubali na naahidi kufuata sheria na taratibu za shule kama zilivyopangwa .Nikienda kinyume nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Tarehe ……………………………… ………………………………

Jina na sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe 20.05.2021 ………………………………

Sahihi ya Mkuu wa Shule MKUU WA SHULE MAKIBA SEKONDARI

Mimi Mzazi/ Mleziwa ………………………………… nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo motto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo

Tarehe ……………………………… Jina na sahihi ya Mzazi/ Mlezi……………………………

Tarehe ……………………………… Jina na sahihi ya shahidi…………………………………

Tarehe 20.05.2021 Sahihi ya Mkuu wa shule …………… MKUU WA SHULE MAKIBA SEKONDARI

Scanned with CamScanner

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MAKIBA SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Makiba Secondary School.

Full name ------------------------------------------------------------------------

Age: ------------------------------------------------------------------------

1. "AIDS' Test ------------------------------------------------------------

2. Blood count (red & white) ------------------------------------------

3. Urine examination ------------------------------------------------

4. Stool examination ------------------------------------------------

5. Syphilis test ------------------------------------------------------

6. T.B Test ----------------------------------------------------------

7. Ear Test ----------------------------------------------------------

8. Eye Test ----------------------------------------------------------

9. Spleen Test ---------------------------------------------------------------

10. Abdomen Test---------------------------------------------------------------

11. Additional information or any other physical, mental, hereditary or intoxication diseases.

-------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------

(Please state nature of treatment)

.......................................................................................................................................

...........................................................................

I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ not to pursue further education.

Signature ------------------------------------------

Designation ----------------------------------------

Station ---------------------------------------------

Date: -------------------------------------------------------

Official stamp ------------------------------------------------ -------------------------------

MKUU W SHULE
MAKIBA SEKONDARI